
# Semina ya Vijana

## 22 August 2022

# Maisha ya kutegemea

# na

# Maisha ya kujitegemea



**Kutegemea**

Watoto chini ya miaka 18

- Chakula
- Mavazi
- Masomo
- Malezi
- Matumizi mengine

**Kujitegemea**

Watu wazima zaidi ya miaka 18

- Chakula
- Mavazi
- Masomo
- Malezi
- Matumizi mengine



# Maandiko Matakatifu yanasema nini…

“Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja” Mwa 2:24

“Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe na mavumbini utarudi” Mwa 3:19

# UTARATIBU WA MAISHA

## MIAKA 0-5 — Hali ya kutegemea sana katika kuishi na kuwa na afya nzuri

- Lazima wazazi wawe makini katika ulinzi, chakula, afya na elimu ili mtoto aweze kukuwa vizuri
- Wanaotelekezwa katika kipindi hiki wengi wanakufa, kuwa walemavu, au wana makovu mengi ya kimwili na kisikolojia

## Miaka 6-20 — Kipindi cha makuzi na mapokeo

- Kipindi hiki ni muhimu sana katika mstakabali wa mwanadamu. Hapa ndipo tunapojifunza mema na mabaya, fani mbalimbali, kujitambua na kuweka msingi wa maisha ya baadae.
- Wanaotelekezewa kipindi hiki huishia kuwa watu maskini na tegemezi katika jamii, au waarifu.

## Miaka 21-39 — Kipindi cha kukuwa kiakili, kiroho, kitaaluma

- Katika kipindi hiki, mwanadamu anapaswa kuvuta uwezo wake wote na kujua kiasi chake katika mambo yote ya kiroho, kimwili, kiakili, kitaaluma na hasa katika kujenga msingi imara wa uchumi wake. Hapa pia mwanadamu utambua na kuchagua wito aidha wa maisha ya ndoa, upadre, utawa au upweke.

# KUJITEGEMEA

- Mtoto anazaliwa akiwa dhaifu kiasi cha kutokuweza kujitegemea kwa lolote isipokuwa kupumua tu



- Mtoto akiachwa bila matunzo ya mama hawezi kuishi
- Sisi wote tupo hai kwa sababu wazazi wetu waliwajibika
- Mama alituosha, akatulisha, kubadilisha nguo, kujali afya, usalama wetu, siku nyingi alikesha, nk. Baba alimsaidia mama.
- Tuna kila sababu ya kumshukuru mama


Kadiri tulivyoendelea kukuwa tulianza kujitegemea


- Kutembea wenyewe
- Kuweza kula wenyewe
- Kwenda haja wenyewe
- Kujivisha wenyewe
- Kuongea
- Kuelewa taratibu
- Kujilinda na hatari ndogondogo kama moto
- Kujitambua kama wa jinsia ya kike au kiume



Katika elimu wazazi na waalimu walichangia pakubwa

- Kutambua maandiko
- Kuweza kusoma, kuandika na kuhesabu
- Kuelewa maana ishara mbalimbali
- Kuweza kutumia tuliyosoma katika maisha ya kila siku kama vile kutumia pesa kwenda kununua vitu dukani
- Kutofautisha vitu kama vile wanyama
- Kupata ujuzi wa kupata hata ajira
- Kutumia elimu kujasiriamali, nk


Faida ya Elimu
Kujali
kujitambua
Kuweka akiba
Kutatua shida
kuwekeza
usikivu
Kung'amua
kuwajibika
Tabia njema
Kutunza mazingira
Uzoefu
Ukarimu
kutangamana



Ukosefu wa elimu
kutojali
kutojitambua
Kutoweka akiba
kukwama
kutowekeza
Kiburi
Kutong'amua
kutowajibika
Tabia mbaya
Kutotunza mazingira
Ujinga
Ubinafsi
kutotangamana

# Mtoto umuleavyo …

# Ndivyo akuavyo




Kama unapenda kudanganya labda mzazi wako alikuwa anapindukia adhabu ulipokuwa unakosea




Kama wewe ni msiri labda mzazi alikuwa anakukemea mbele za watu ukikosea




Kama unatabia ya kujibu vibaya au kofoka itakuwa uliipata kwa wazazi au watu uliolelewa na au mazingira ulimokulia




Kama unakasirika haraka itakuwa haukupongezwa kwa lolote ulipokuwa mdogo na ulikasirika ili kuonekana




Kama haujiamini kwa lolote itakuwa ulikuwa unaelekezwa tu bila kupewa nafasi ya kuamua chochote




Kama wewe ni mvivu na mwoga itakuwa ulifanyiwa kila kitu na wazazi au ndugu wakubwa

# Imani na maisha ya imani

- Imani ni dhana pana sana.
- Imani ni dhihirisho la matumaini yanayopita dhamiri ya akili na tafakari ya mwanadamu.
- Imani ni kitu tunachorithi kwa wazazi, walezi, walimu na jamii inayotozunguka.
- Imani ni jambo muhimu na nyeti sana linalopaswa kuchukuliwa kwa umakini mkubwa
- Mtu ambaye hana msimamo dhabiti wa imani huwa anayumba sana katika kila jambo

# Aina za imani

- Imani kwa nafsi – uwezo wa kusadiki kwamba mimi naweza kufanya mambo Fulani na kufanikiwa
- Iani kwa ndugu – kwamba ndugu zangu hawazezi kunitendea lolote baya
- Imani kwa marafiki – kwamba rafiki zangu hawawezi kunisaliti
- Imani kwa jamii – kwamba jamii yangu inanitambua na kunilinda
- Imani kwa serikali – kwamba serikali inajali masilahi yangu
- Imani kwa wengine – dereva, waalimu, walinzi, wapishi, etc.
- Imani kwa Mungu – Kwamba Mungu yupo, ndiye aliyeniumba, ananipenda na kujali maisha yangu, ananisaidia na nikifa nitarudi kuishi naye milele

# Matokeo ya kuwa na imani

- Imani ni lugha ya nafsi ya mwanadamu
- Imani inadhibiti mtazamo wetu wa maisha na jinsi tunavyotangamana na mazingira na watu wanaotuzunguka
- Imani inatusukuma kufanya mambo fulani na kutuzuia kufanya mambo fulani
- Imani inadhibiti tabia ya mtu katika mambo ya binafsi na mambo yanayohusu wengine

- Imani nzuri inachangia amani, maendeleo, ufanisi na uendelevu wa mtu binafsi na jamii kwa jumla.
- Watu wanaoishiriki imani moja wanaweza kushirikiana kwa mambo mengine katika jamii hivyo kuleta maendeleo kwa wote.
- Tofauti za kiimani zinaweza kusababisha chuki, utengano na hata madhara kati ya makundi tofauti
- Imani potovu ni hatari sana katika maisha ya mtu binafsi na kwa jamii nzima
- Kila imani ina taratibu zake ambazo zinamhitaji muumini kuzifuata ili apate mafanikio yanayoendana na imani husika
- Imani inaweza kuwa chombo cha uovu, utapeli, au kupanga na kutekeleza malengo fulani.

- Imani inajengwa kwa kushawishi
- Watu walio na ujuzi na kipaji cha kuwashawishi watu anaweza kuwavuta kuamini chochote
- Watu wengi wamewekeza katika ujuzi wa kushawishi
- Imani inaweza kumfanya mtu aweze kufanya mambo ambayo hakuyatarajia (Mk 9:23) kila kitu kinawezekana kwa imani.
- Imani inaondoa uoga na kukata tamaa
- Imani ni njia ya kutafuta suluhu ya changamoto
- Imani pia inaweza kutumiwa vibaya kuchochea chuki au vita na ugaidi


# Kujasiriamali

- Kujasiriamali jambo la maana zaidi ambalo mwanadamu anao uwezo wa kufanya kwa kujiamini
- Wajasiriamali ni watu ambao wana ujasiri mkubwa na moyo wa kufanya kazi bila kujali kuchoka
- Uwezi kufanikiwa katika maisha bila kutoa jasho (Mwa 3:9) “kwa jasho lako utakula”
- Mtu yeyote anayekula na kunywa bila kutoa jasho au kuchoka anakula jasho na uchovu wa watu wengine
- Kutofanya kazi ni hujuma kwa uchumi wa familia, jamii na taifa
- Kila mtu anaweza kufanya jambo moja au jingine hata mlemavu

# Penye nia na moyo pana njia

- Vijana wengi wanasingizia mambo mengi kutofanya kazi
    - Sikusoma
    - Sina hela
    - Sina mtaji
    - Sina wazazi
    - Babangu ni mlevi
    - Watu hawanipendi
    - Hamna kazi
    - Hamna fursa
    - Hamna hamna nk


ntv


ktn NEWS
KTN PRIME
SMS 22155
MUTHAMA IN HOT SOUP
PARTY ACCUSES HIM OF MISCONDUCT
9:24:03 PM
BRIEFS
e was unthinkable, says Klopp | Justin Kluivert offered t



# kuwezeshwa

- Kuna watu wengi waliochangia sana na bado wanachangia zaidi katika maisha ya kila mmoja wetu
- Njia nzuri zaidi ya kurudisha mkono ni kuwawezesha wengine pia kujitambua na kufikia malengo yao
- Ukarimu unavuta ukarimu kila wakati, ubinafsi unaleta umaskini wa utu.

# Sasa tufanyeje

- Usisubiri kufanyiwa kila kitu
- Ni muhimu kuanza kwanza alafu kuomba mawazo na msaada kwa wale ambao unaona wana uwezo wa kukusaidia
- Swali ni je! Ni nini ambacho naweza kufanya?
- Usikubali kukashifiwa na watu ambao hauwezi kuwaomba ushauri. Hao wana nia ya kukusaidia ila kukuvuta nyuma

Imeandaliwa na

Fr. Lawrence Muthee, SVD